JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHAMA KWA OFISI ZA MAKAO MAKUU YA TCU - DODOMA

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kuwafahamisha wadau na wananchi kuwa Ofisi za Makao Makuu ya Tume, ambazo awali zilikuwa katika Jengo la SUMA JKT, Mtaa wa Tambukareli, Dodoma, zimehamia katika Jengo la Makao Makuu ya TCU lililopo **Kisasa B, Kiwanja Na. 56/4, Kitalu E, Barabara ya Ilazo, 2 Mtaa wa TCU, 41220 Nzuguni, Dodoma.** Kuanzia sasa huduma zote zinazotolewa na Ofisi za Makao Makuu ya TCU zinapatikana katika eneo hilo. Hivyo, mawasiliano yote yanayohusu TCU yawasilishwe kupitia anuani ifuatayo:

Katibu Mtendaji,
Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),
S. L. P 2600,
**DODOMA.**

**Simu:** +255 (0)26 2161560 / +255 (0)26 2161561
**Barua pepe:** es@tcu.go.tz

Aidha, TCU inapenda kuwafahamisha wadau na wananchi kuwa huduma zake zitaendelea kutolewa pia kupitia Ofisi za TCU zilizopo Dar es Salaam katika Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mtaa wa Magogoni.

TCU inawashukuru wadau na wananchi kwa ushirikiano wao na inaahidi kuendelea kutoa huduma bora kwa ufanisi na kwa wakati.

Imetolewa na:

**Prof. Charles D. Kihampa**
**KATIBU MTENDAJI**
10/8/2026